

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



NA. 21 YA 1982

NAKUBALI,

2: Novemba, 1982

Julius K. Nyerere
Rais

**Kufanya mabadiliko katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano
kwa madhumuni ya kuweka utaratibu mpya wa uteuzi wa Wakuu
wa Mikoa**

[.....]

IMETUNGWA na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

1. Sheria hii iitwe Sheria ya Mabadiliko ya Nne katika Katiba ya Nchi, na itanza kutumika tarehe 1 Novemba, 1982.

Jina la
Sheria na
tarehe ya
kuanza
kutumika

2. Ibara ya 19 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya mwaka 1977, inafanyiwa mabadiliko kwa kuifuta ibara ndogo ya (1) ya ibara hiyo na kuweka badala yake ibara ndogo ifuatayo: —

Mabadiliko
katika
ibara ya
19 ya Katiba

“(1) Kutakuwa na Mkuu wa Mkoa kwa kila mkoa katika Jamhuri ya Muungano, ambaye atateuliwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.”.

Ninathibitisha kuwa Muswada kwa ajili ya Sheria hii umepitishwa na Bunge kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 52 (1) (a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya Mwaka 1977.

A. S. MKWAWA,

A. S. Mkwawa
Spika

Imepitishwa katika Bunge tarehe 15 mwezi wa Oktoba, 1982.

[Signature]
Katibu wa Bunge